Kabla ya

KUOMBA

Maombi ni zaidi ya mbwemwe!

Shemeji

Melayeki

KABLA YA KUOMBA © 2019 Shemeji Melayeki

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi isipokuwa kwa nukuu mbalimbali na matumizi ya kufundishia.

SIMU: +255 714 548 565

+255 763 965 297

Email: *shemeji.melayeki@gmail.com*
YouTube: *Shemeji Melayeki*
Instagram: *apostle_shemeji_melayeki*
Twitter: *@melayeki*
Facebook: *Ap Shemeji Melayeki*

ISBN - 987-9976-5427-6-9

Kimepigwa chapa na: ***CLIMAX SOLUTIONS – ARUSHA***

+255 658 288 054

+255 687 699 862

+255 763 965 297

YALIYOMO

TABARUKU iv

SHUKRANI v

DIBAJI vi

MAONI YA WANAFUNZI vii

MAOMBI SIYO SARAKASI 1

Siyo Unavyojisikia Wakati Wa Maombi 2

Siyo Unavyojisikia Baada Ya Maombi 2

Siyo Urefu wa Muda Wa Kuomba 3

Siyo Ukubwa Wa Sauti Ya Mwombaji 4

Siyo Pozi La Kuombea 6

Siyo Mahali Unapoombea 7

Siyo Idadi Ya Watu Wanaoomba 8

Siyo Idadi Ya Maandiko Kwenye Maombi 10

MAOMBI 12

MTAZAMO WA MWOMBAJI JUU YA MUNGU 12

MOYO WA MUNGU 13

KUOMBA KWA IMANI 18

MAOMBI YA HANA 29

IMANI KUBWA AU HABA? 31

KUMWENDEA-ENDEA MUNGU 42

MUNGU HACHELEWI 45

KIPI KILICHO KIGUMU? 49
HAYA NI MAPENZI YA MUNGU 54
MFANO WA BABA MWOVU 56
YO YOTE MYAOMBAYO 58
NIA YA MWOMBAJI 60
MTINI ULIOLAANIWA 66
Vitabu vingine vya Shemeji Melayeki 72

TABARUKU

Kwa mke wangu Neema, hatua za mwanzo za uhusiano wetu ilinipa darasa la kutaka kumjua Mungu zaidi.

Kwa jamii ya waaminio wanaozungumza lugha ya Kiswahili, wenye kiu ya kuifahamu kweli ya Kristo, kutazama mambo kwa jicho la Kristo na kuona uhusiano wao na Mungu ambaye ni Baba yetu unakuwa imara kila siku.

SHUKRANI

Kwa Mungu ambaye ni Baba wa roho zetu na mwasisi wa maisha tuliyonayo, nakushukuru kwa utulivu wakati wa kukiandaa kitabu hiki.

Kwa familia yangu, mara nyingi nimekuwa macho usiku wakati wamelala, kwa utulivu mkubwa walionipa. Mke wangu amenifanya nitamani kujua zaidi urahisi uliopo katika maombi yake. Ilikuwa inanisumbua kusikia *"Jana nilimwomba Mungu anipe surprise. Yeye si Baba yangu bhana."* Mara utasikia *"Nataka Mungu anitoe out".* Sikuwahi kufikiri mtu anaweza kuwa na uhusiano na Mungu kwa kiasi hicho. Lakini shuhuda zake zilikuwa zinasumbua mtazamo wangu juu ya maombi. Kitabu hiki ni zao la kutaka kujua nisichokijua kuhusu maombi yake.

Kwa timu ya watu waliojitolea kujifunza kupitia kwangu kwenye huduma ya Global Family Gatherings Na wengine wengi kwa njia ya mitandao ya kijamii, wamekuwa sababu ya kunifanya nijitume

zaidi ili kila asubuhi wakute mlo ukiwa wa moto.

Kwa wadau wanaofanya huduma pamoja na mimi kwa njia ya sadaka zao ili kuhakikisha kazi hii haikwami, wamekuwa waaminifu kwa rasilimali zao ili kweli hii ienee zaidi.

DIBAJI

Kati ya jambo linalofanywa sana na watu wengi, si wakristo tu peke yao ni maombi. Wakati fulani nilikuwa nafikiri naelewa vizuri juu ya mambo yahusuyo maombi. Si hivyo tu ukipima uombaji wa watu wengi na matokeo ya maombi hayo unaweza kushangaa sana. Mtu mmoja alisema kama maombi yana matokeo basi wanamaombi wangekuwa na maisha mazuri kuliko watu wengine wote. Mtu kuwa kwenye kikundi cha maombi haina maana anamwamini Mungu na anapokea kitu kutoka kwa Mungu. Kitabu hiki hakifundishi mbinu au hatua za kuomba kwani vitabu vya aina hiyo tayari vipo na si vitabu tu kuwepo lakini watu wengi tayari wanazo mbinu nyingi sana za kuomba.

Lengo langu hasa ni kukufunulia moyo wa Mungu, Baba yetu anavyotutazama juu ya yale tuyaombayo

na kuujua hakika moyo wake. Hii itakuwa rahisi sisi kujenga mahusiano yaliyoshikiliwa na kweli iliyofunuliwa katika kitabu hiki.

MAONI YA WANAFUNZI

Haya ni maoni ya wanafunzi waliojifunza mfululizo wa masomo haya kuhusu maombi kwa njia ya Whatsapp.

Maombi yanategemea sana hali ya mwombaji juu ya yule anayemwomba. Mwombaji anapaswa kujua kuwa Munguni mwaminifu na anataka kumjibu maombi yake siku zote, yeye habadiliki kwahiyo anayepaswa kubadilika ni mwombaji, huyo ndiye Mungu sifa yake ni mwaminifu kuwa atatupa yale tuliyomwomba.

Mtazamo sahihi juu ya Mungu unaamua kiwango cha ubora wa matokeo kwenye maombi kwa sababu usahihi wake utaamua usahihi wa imani ambayo ndiyo njia ya kupokea kutoka kwa Mungu. Maombi sio ushawishi wako kwa Mungu kwa

maneno mengi na sauti kubwa bali ni kumimina moyo wako kwa imani na kumtegemea kuwa yale uliyomwomba ameyasikia na ameyajibu na ndivyo alivyo siku zote. Kama baba zetu wa dunia wanapenda kutusikiliza na kutupa mahitaji yetu basi Mungu ni zaidi kwa sababu anatupenda na kutujali kuliko baba zetu na tukiweka tegemeo letu hapo na pumziko amani ya Mungu itatufunika na tunajua tunazo tayari zile haja zetu tulizomwomba.

Ebenezer Asanterabi Shoo

Kama mwombaji anayetarajia maombi yake yawe na matokeo, swala la mtazamo wa mwombaji juu ya Mungu ni jambo la muhimu sana. Ndani ya mtazamo kuna vitu kadhaa ambavyo mwombaji anatakiwa awe na uhakika navyo. Mtazamo wake juu ya Mungu unaamua imani yake juu ya Mungu; kuamini nafasi ya Mungu katika kuleta matokeo na kuamini katika kile unachokiomba. Kama ufahamu wako upo sahihi juu ya Mungu, imani yako itakuwa thabiti na matarajio yatajengeka ndani yako yatakayozaa matokeo katika kile ulichoomba na ndani ya ufahamu wako unatakiwa kujua kwamba katika maombi unayofanya, kinachotakiwa kuingia na kubaki kwenye ufahamu wako ni UKUU na UWEZA wa Mungu tu ndio unaodumu.

Rahel Lotas Hagai

Afisa Rasilimali watu.

Mfanyakazi - Smile Communications.

Nilikuwa naona kuomba mpaka upitie michakato kadhaa ndiyo Mungu asikie. Nilikuwa mwepesi wa kujihesabia haki na pia kuhukumu wengine na kuona kuwa Mungu hawezi kuwasikiliza kwa sababu hawazijui kanuni za kumwendea Mungu. Kuna wakati nilikuwa nashindwa kuomba pia kwa kudhani Mungu hawezi kunisikia wala kunisamehe tena. Lakini nimejifunza kuwa Mungu hajawahi kumuwazia mtu mabaya ikiwa ni pamoja na mimi.

Eneo hili la imani pia nilikuwa naona kuna mambo Mungu anaweza kufanya ila mengine hawezi (japo ninaimba kila siku hakuna lisilowezekana kwa Mungu).

Justina Reuben

Maombi ni zaidi ya muda unaotumia kuomba, idadi ya watu, aina au sauti unayotumia ambavyo. Lakini jambo la msingi ni mtazamo wako sahihi juu ya Mungu ambao unaleta imani kubwa kwa Mungu. Mwombaji anatakiwa kujua kuwa Mungu ni pendo, anatupenda na yuko tayari kutatua matatizo yetu.

Severina Gabriel

Mwandishi

Wakati wowote ule na mahali popote pale unaweza ukaomba na kupata matokeo. Katika kuomba maombi yenye matokeo kwa Mungu wetu kuna mambo lazima tuyajue vizuri sana. Mtazamo kuhusu Mungu wetu kwa kuutazama UAMINIFU WAKE NA WEMA WAKE una nafasi kubwa sana ya kuiachilia imani zetu ili tupate matokeo ya maombi. Kuomba kwa Imani kunaleta uhakika wa kupokea kutoka kwake, bila kujali hisia unazopata baada ya maombi.

Hassan Adam Mlimbila

Mwanafunzi - Chuo Kiku cha Dar es salaam

Maombi ni Matokeo ya kuwa na imani kwa yule ninayemwomba (MUNGU) pekee na kuamini nimeshapokea ninachokiomba!

Siyo muda niliotumia kuomba,siyo idadi ya Maandiko ya Biblia ninayoyafahamu,siyo mahali lipoombea, wala siyo sauti yangu kubwa wakati ninaomba! tena siyo nnavyojisikia wakati ninaomba au baada ya kuomba. Kabisa siyo idadi ya watu ambao ninaoomba nao bali ni KUOMBA KWA IMANI.

Kumwamini yule ninayemwomba (Mungu) kuwa

ndiye HAKI YANGU na ANAJIBU UPESI. Sihitaji kumwendea MUNGU nikiwa na mtazamo wangu huku nikijihesabia haki/kujistahilisha kwa mambo niliyoyafanya nikiwa ninaomba!

Angelina Shoo.

Rural Development Expert and Children Program Specialist.

Unaweza ukaomba kwa masaa mawili tena maombi ya mfungo usijibiwe lakini aliyeomba maombi kwa dakika mbili katika IMANI akapata majibu. Mungu ni mzuri anasubiri useme tu ukiamini yeye ni mpaji pasipo shaka yoyote ili akupe- furaha yake ni kuwapa watoto wake haki yao, anafanya kwa ajili ya jina lake sio kwa kujihesabia haki. majibu ya maombi sio kwa sababu ya kazi fulani njema sana uliyofanya kwa Mungu bali ni kwa neema tu na kwa sababu mungu anatupenda sana na anatupa kwa sababu anafurahia furaha yetu.

Joshua Ibrahim

Uyole Mbeya

Ili nipate matokeo jambo la msingi ni kuwa na MTAZAMO SAHIHI juu ya huyu mleta matokeo. Natakiwa kufahamu kuwa Yeye ni BABA mimi ni MWANA na naweza kuwasiliana naye mahali

popote, muda wowote vyovyote. Natakiwa kumwamini na kufahamu kwamba maombi sio tool ya kutuliza stress, hofu na hisia zangu. Maombi ni njia ya mazungumzo na Baba yangu anayejua ninayohitaji hata kabla sijamuomba. Sio lazima kutiririsha Bible verses nyiiingi au kutoa sauti mpaka ikauke ili alete matokeo. Kama vile mtoto anavyooomba Biscuit akiwa mikononi mwa baba yake ndivyo natakiwa kumwomba Mungu kwa KUNYENYEKEA mikononi mwake nikijua kuwa yeye ni Baba yangu na hata matokeo yasipoonekana ghafla bado najua ameshafanya kwa kuwa ni mwema.

Danford Marco

Textiles and Graphics Designer

Sio hali yangu ya uduni ama mazingira niliyonayo yanayosababisha kujibiwa kwa maombi yangu isipokuwa ni vile Mungu alivyo na ukuu wake katika kutenda mambo ya ajabu. Kwa neema yake Mungu anatustahilisha vile hatukustahili. Maana Bwana kama angehesabu maovu yetu nani angesimama. Hivyo tunavyojibiwa sio kwa sababu ya utakatifu wetu bali ni neema yake juu yetu. Kuweka tumaini letu kwa 100% kwenye uaminifu wake ni jambo la muhimu sana sana. Hivyo maombi ni zaidi ya mtindo wa kuomba bali imani yetu katika uaminifu

wa Mungu Baba yetu.

Maria Mtili, Dar es Salaam

MAOMBI SIYO SARAKASI

Maombi ni matokeo siyo matukio. Maombi ni majibu na si vinginevyo. Kama unaomba maombi ya kutaka kusaidiwa na Mungu kushughulikia jambo fulani; kama hilo jambo halipati ufumbuzi, sarakasi zote kwenye maombi ni ubatili na kujilisha upepo. Maombi yamekuwa na staili nyingi na mbwembwe nyingi sana. Changamoto ni kwamba imefika hatua ni kama watu wanaabudu mbinu na *styles* za kuomba kuliko anayeombwa. Kwa hiyo watu wengi sana wameondoka kwenye kiini cha maombi. Ukichunguza kwa makini utagundua, idadi ya watu wanaoomba ni wengi kuliko wanaopata majibu na matokeo yanayoshikika. Ni ukweli unaoumiza nikikwambia *"kuna watu wengi wanafanya matukio yanayoitwa maombi bila majibu"* Je, kiasi cha majibu au matokeo ya maisha yako yanafikia nusu

ya maombi yako? Ikiwa Yesu aliweka wazi, *ombeni nanyi mtapewa,* sasa shida iko wapi? Je, ni kwamba hawapokei? Kama hawapokei; tatizo liko wapi?

Siyo Unavyojisikia Wakati Wa Maombi

Kuna wakati nilikuwa nikiomba kuna hali fulani naitafuta kwenye maombi ili nijue kama niko vizuri kusikiwa na Mungu au la. Wakati fulani nilikuwa natafuta namna fulani ya kujisikia wakati naomba kama sipati ninaanza aidha kutuba (kwamba pengine kuna jambo baya nimefanya) au hata badala ya kupeleka hoja zangu kwa Baba yangu ninaanza kubomoa anga la sehemu hiyo (nikidhani labda kuna ugumu kwenye anga) hata kama ni chumbani kwangu wala sijali kama jana nilibomoa tena anga hilo hilo. Utasikia mtu akisema maombi ya leo yalikuwa na nguvu sana kwa sababu ama alianguka wakati wa maombi au alijisikia kulia, aliona sehemu ya mwili ikitetemeka, aliona vitu asivyovielewa alipofunga macho na jumla ya hisia mbalimbali. Pamoja na hayo yote kama matokeo hakuna hilo nalo ni kazi bure.

Siyo Unavyojisikia Baada Ya Maombi

Wengine huenda mbali zaidi kwa kutaka wapate hali fulani baada ya maombi, hapo wanajisikia vizuri kwamba hapo sasa wameomba, bila kujali ameomba nini. Umewahi kusikia mtu akisema

nilipotoka kwenye maombi nilijisika mwepesiiiii. Kuna wakati kwa ajili ya uchanga wangu, nikiomba natamani nisikie hali fulani au uzito kifuani. Nikiona hivyo naona maombi yalikuwa *fire* sana. Utashangaa sana kugundua kuwa watu wanaomba ili wajisikie vizuri tu, ni kama wanasema *kwa kweli nashukuru nimeomba.* Wakati watu wanasafiri kwenye vyombo vya usafiri, ukijua kinachowafanya waombe utashangaa sana. Watu wengi katika safari zao wengi hawaombi kwa sababu wanamwamini MUNGU ila ni kwa sababu wanaogopa ajali. Hiyo inaweza kuwa msukumo wa maombi. Kwa hiyo motivation yao ni hofu ya kufa siyo ukuu na uweza wa Mungu. Hivyo akiomba anajisikia vizuri. Siku ya kwanza napanda ndege kwa kweli nilifanya maombi yote ninayoyajua ya kuomba msamaha. Nilikuwa na hofu kuu, nilifikiri nikiomba angalau nitajisikia vizuri safarini. Nilichokuwa nataka kwa kweli ni kuondoa *stress* niliyokuwa nayo kwenye ndege. Maombi haya siyo kwa sababu kuna uhakika na ulinzi wa Mungu bali jitihada za kujiandaa kwa hali zote. Lakini maombi yanaweza kabisa yakawa ni biashara ya kutuliza hofu wala siyo kwa sababu unaamini utapata matokeo.

Siyo Urefu wa Muda Wa Kuomba

Kuomba muda mrefu ni jambo zuri, lakini haiamui majibu kabisa. Kuna wengine waliomba muda mfupi tu wakapata matokeo, wengine hata wakifunga bado hawapati matokeo yoyote na hawajui tatizo liko wapi. Wengine huenda mbali kwamba kama hujaomba kwa saa moja na zaidi hili halitawezekana. Kwa lugha rahisi muda wa maombi umekuwa na nguvu kuliko anayeombwa. Maombi mafupi kama "*nisaidie*" Mungu pia huyajibu. Kwamba yawe ya siku arobaini au ya sekunde kumi, Je, kuna matokeo? KAMA HAKUNA MATOKEO BASI KUNA KITU HAKIKO SAWA…

Siyo Ukubwa Wa Sauti Ya Mwombaji

Niliwahi kukaa sehemu ambapo kuna kanisa karibu. Muda wa maombi hata kama mtu yuko peke yake anawasha vyombo vya muziki vyenye spika zenye sauti kubwa lakini changamoto ni mambo anayoyaombea. Nilikuwa namsikiliza halafu naishia kusema *"hata akijibiwa hajui amejibiwa jambo lipi!"*

Hana aliomba na sauti yake haikusikika lakini tunaona matokeo ya maombi yake (Samweli) yalionekana wazi. Hata wakati anaomba kwa jinsi alivyokuwa anaomba kuhani akafikiri pengine amelewa. Kama lengo lako ni kusikika (ukishasikika) basi umeshapokea thawabu yako wala huwezi

kupata kitu kingine kutoka kwa Mungu. Lengo lake halikuwa kuonekana na kuhani jinsi alivyo hodari katika kupanga maneno wakati wa maombi bali alimimina moyo wake kwa Bwana. Ni afadhali kumimina moyo wako kwa Bwana kuliko kusambaza maneno yaliyojaa unafiki. Wakati tunaongoza maombi kwenye mikusanyiko yetu tunawaambia watu waongeze sauti na kutokuelewa kwao wakaanza kufikiri maombi ni muhimu yaambatane na sauti ya juu. Hata leo kuna watu wakiambiwa wapunguze sauti wakati wa kuomba wanakuona umerudi nyuma kabisa. Kuna wakati nilikwenda kutafuta ukumbi wa kufanyia ibada kwenye hoteli moja wakapata sana shida kwani pale wanalala wageni. Nikawauliza sababu inayowafanya waogope kutupatia ni kwa sababu tulisema tu *"tunataka kufanya semina za kiroho"?* Sababu kubwa waliwahi kuwapa watu ukumbi lakini kelele zilikuwa nyingi wakati watu walikuwa ndani hawakuzidi kumi na ilileta usumbufu mkubwa. Watu hawa wakiambiwa wapunguze sauti mara nyingi huwaona wengine siyo wa kiroho na hata hutishia kuhama. Huu ni ulimbukeni wa kiwango cha PhD.

Ndugu mmoja aliwakuta watu wanakemea pepo ndani ya mtu kwa muda zaidi ya saa tatu. Utawakuta wapendwa walikunywa maji mpaka wakachoka, wakahisi wao ndio wenye shida wakaanza kutubu na kujitakasa, haikutosha wakaanza kutubu juu ya dhambi za ndugu mwenye mapepo na ukoo wa pia bila matokeo. Haikutosha, nguo zilikuwa zimelowa kwa kumnywesha maji huku wakisema *"Kunywa hiyo ni damu ya Yesu"* alipofika akawauliza, *"mbona mnahema hivyo?"* Wakamjibu *"hili ni saa la tatu pepo halitoki".* Akawauliza shida ni nini, wakasema *"hili pepo ni lile sugu"* akashangaa kwamba wanaamini kuna pepo haliwezi kutoka kirahisi. Yaani unaweza kufikiri hawa ni wakristo au manabii wa Baali. Yule ndugu alipomwangalia yule mgonjwa akiwa anakoroma, akasema kwa hasira *"Pepo toka na usimrudie tena"* yule aliyekuwa amepagwa akafungua macho na kuamka. Sasa kupaza sauti siyo jambo baya hasa kama uko kwenye mazingira ya kutowabughudhi watu, lakini kufikiri Mungu anatumia kigezo hicho kujibu au kutokujibu ni

moyo wako kwa Bwana kuliko kusambaza maneno

kuupotezea uhalisia juu ya moyo wa Mungu. Kama hakuna matokeo tutakauka koo tu bure.